**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 09 Septemba, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 24 Juni, 2026.

1. Toleo Namba 7490 la tarehe 16 Aprili, 2026
2. Toleo Namba 7468 la tarehe 08 Mei, 2026
3. Toleo Namba 7472 la tarehe 08 Mei, 2026
4. Toleo Namba 7469 la tarehe 08 Mei, 2026
5. Toleo Namba 7470 la tarehe 08 Mei, 2026
6. Toleo Namba 7471 la tarehe 08 Mei, 2026
7. Toleo Namba 7477 la tarehe 15 Mei, 2026
8. Toleo Namba 7478 la tarehe 29 Mei, 2026
9. Toleo Namba 7482 la tarehe 15 Mei, 2026
10. Toleo Namba 7483 la tarehe 22 Mei, 2026
11. Toleo Namba 7474 la tarehe 29 Mei, 2026
12. Toleo Namba 7475 la tarehe 29 Mei, 2026
13. Toleo Namba 7476 la tarehe 29 Mei, 2026
14. Toleo Namba 7479 la tarehe 29 Mei, 2026
15. Toleo Namba 7480 la tarehe 29 Mei, 2026
16. Toleo Namba 7481 la tarehe 29 Mei, 2026

17. Toleo Namba 7487 la tarehe 05 Juni, 2026
18. Toleo Namba 7495 la tarehe 19 Juni, 2026
19. Toleo Namba 7496 la tarehe 03 Julai, 2026
20. Toleo Namba 7498 la tarehe 30 Juni, 2026
21. Toleo Namba 7499 la tarehe 30 Juni, 2026
22. Toleo Namba 7500 la tarehe 01 Julai, 2026
23. Toleo Namba 7502 la tarehe 01 Julai, 2026
24. Toleo Namba 7496 la tarehe 03 Julai, 2026
25. Toleo Namba 7501 la tarehe 03 Julai, 2026
26. Toleo Namba 7504 la tarehe 17 Julai, 2026
27. Toleo Namba 7505 la tarehe 17 Julai, 2026
28. Toleo Namba 7506 la tarehe 17 Julai, 2026
29. Toleo Namba 7507 la tarehe 17 Julai, 2026
30. Toleo Namba 7508 la tarehe 17 Julai, 2026
31. Toleo Namba 7509 la tarehe 24 Julai, 2026
32. Toleo Namba 7510 la tarehe 24 Julai, 2026
33. Toleo Namba 7512 la tarehe 31 Julai, 2026
34. Toleo Namba 7513 la tarehe 31 Julai, 2026
35. Toleo Namba 7514 la tarehe 07 Agosti, 2026
36. Toleo Namba 7515 la tarehe 07 Agosti, 2026
37. Toleo Namba 7516 la tarehe 07 Agosti, 2026
38. Toleo Namba 7518 la tarehe 14 Agosti, 2026
39. Toleo Namba 7519 la tarehe 14 Agosti,2026

**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga Upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa Madhumuni ya Kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga Upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa Madhumuni ya Kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

200. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Nam. 1 ya 2015, Kamati za Maafa za Wilaya na Shehia, zina jukumu pamoja na mambo mengine, kuhamasisha na kutafuta rasilimali za kifedha na nyenzo nyingine kwa ajili ya kujiandaa na kukabiliana na maafa katika maeneo yao.

(a) Je, Shehia saba za Wilaya ya Chake Chake zimehamasisha au zimekusanya kiasi gani cha fedha kwa ajili ya usimamizi wa maafa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

(b) Je, Kamati ya Maafa ya Wilaya ya Chake Chake imehamasisha au imekusanya kiasi gani cha fedha katika kipindi hicho, na fedha hizo zimetumika katika shughuli zipi.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

10. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Moja ya changamoto inayowakabili vijana wetu wengi wa Zanzibar ni Utumiaji wa Dawa za Kulevya na Pombe.

(a) Ni watuhumiwa wangapi wa dawa za kulevya wamekamatwa kwa kipindi cha mwaka 2025-2026.

(b) Kwa kiwango kipi Serikali inatambuwa malalamiko ya kuteswa kwa raia wasiokuwa na hatia katika kambi za askari za Dawa za Kulevya Kilimani na Pujini.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

288. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Baadhi ya viongozi wenye majukumu makubwa ya Serikali wanaendesha gari wenyewe wakati wa utekelezaji wa majukumu rasmi, jambo linaloibua hoja kuhusu upatikanaji wa gari na madereva kwa viongozi wenye stahiki hizo.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapatia gari na madereva viongozi wenye stahiki hizo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao rasmi.

(b) Je, ni viongozi wangapi wenye stahiki ambao kwa sasa hawajapatiwa magari au madereva.

(c) Je, ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha viongozi wenye stahiki wanapatiwa huduma hizo kwa wakati.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

162. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuulliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na uchafu mkubwa sana katika nyumba zetu za Michenzani, unaosababishwa na kujaa kwa makaro pamoja na utupaji taka kiholela.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha uchafu unaondolewa katika maeneo ya Michenzani.

182. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU Nam. 6 ya 2003), Taasisi hiyo imeanzishwa kwa madhumuni ya kuwaandaa vijana wa Zanzibar kupitia mafunzo uzalendo, nidhamu, elimu ya uraia, ulinzi, pamoja na shughuli za uzalishaji mali na maendeleo ya kijamii. Sheria hiyo inaonesha wazi dhamira ya Zanzibar kuwa na mfumo wake wa kuwajenga vijana kwa kuzingatia mazingira, mahitaji na vipaumbele vya Zanzibar.

Ni kwa namna gani Serikali ya SMZ inatekeleza matakwa ya kifungu hiki cha Sheria.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

47. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kutokana na kuwepo hamasa kubwa kwa Vijana katika kutafuta ajira nje ya nchi;

(a) Je, Serikali imepeleka Vijana wangapi hadi sasa kufanya kazi nje ya nchi.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika kusafirisha Vijana hao.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

26. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mfuko wa Huduma za Jamii wa Zanzibar (ZSSF) umekuwa ukipokea fedha za watumishi na kuzihifadhi mpaka pale wanapostaafu. Inafahamika kuwa Mfuko unawekeza fedha hizo ili kuziendeleza katika miradi mbalimbali nchi na hivi karibuni uwekezaji wa fedha hizo za wafanyakazi umeelekezwa katika miradi mingi nchini.

(a) Je, ni miradi mingapi mipya imeekezwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(b) Je, ni faida ya kiasi gani cha fedha imepatika katika miradi ya zamani ya Mfuko.

(c) Je, ni miradi gani ambayo haifanyi vizuri na utaratibu wa kuondokana nayo upo vipi.

280. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Baadhi ya watumishi wanaostaafu, husubiri kwa muda mrefu kupatiwa kiinua mgongo na mafao mengine, hali inayowaathiri kiuchumi baada ya kumaliza utumishi wao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa ucheleweshaji wa malipo ya kiinua mgongo na mafao mengine ya wastaafu.

(b) Je, wastaafu wangapi ambao bado hawajalipwa na jumla ya fedha wanazodai ni kiasi gani.

(c) Je, lini Serikali inatarajia kukamilisha malipo ya stahiki hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

219. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali kupitia Mkopo wa *Exim Bank* ya India, imejenga tangi kubwa la kuhifadhia maji katika eneo la Kwarara, jambo lililopelekea kuwepo kwa maji ya kutosha katika eneo hilo na maeneo ya jirani.

(a) Ni lini Serikali itayafanyia matengenezo ya kudumu mabomba makubwa ya maji yanayopokea maji kutoka tangi la Kwarara na kuyapeleka katika Shehia za Jimbo la Mwanakwerekwe na maeneo jirani, mabomba ambayo yamekuwa yakipasuka mara kwa mara na kusababisha maji kumwagika kwa wingi na wananchi kukosa huduma hiyo.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika bajeti ya mwaka 2026/2027 kwa ajili ya kuimarisha huduma za maji kupitia tangi la Kwarara.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

224. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wanafunzi wanaosoma Shahada ya Uzamivu (Phd) katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), wanalipa zaidi ya milioni kumi na mbili. Wanafuzi hao wakati wanapohitimu masomo yao na kurudi katika Utumishi wao wa Umma, hupata nyongeza kati ya elf 50 hadi 70, na wengi wao wanamaliza wakiwa na deni walilokopa kutoka Bodi ya Mikopoy a Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Zanzibar.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasamehe au kuwafanyia tahafifu wanafunzi hao, ili tupate nafasi ya kuongeza idadi ya wasomi nchini.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

134. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la huduma ya mtandao wa *internet* ya *fiber to home*, ambapo kila Mtoaji Huduma ya *internet* (ISP) anapitisha nguzo mitaani kusambaza *fiber* na kusababisha utitiri wa nguzo mitaani.

(a) Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kunakuwepo na mpangilio mzuri wa usambazaji wa nguzo za *internet* ya *fiber* mitaani.

(b) Je, kwa nini Wizara haitoi muongozo mzuri kwa Watoa Huduma hii kutumia kwa pamoja nguzo moja au kuwa na Mkandarasi mmoja wakujumuisha *fiber-cable* zote katika mfumo wa nguzo moja kama vile katika minara ya simu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

19. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tunaipongea Serikali katika jitihada zake za kukusanya mapato kwa kutumia Mifumo ya Kielektroniki hasa mapato ya maegesho katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar. Hata hivyo, baadhi ya watendaji wa maeneo ya maegesho wanashindwa kusimamisha muda kwenye mfumo wakati gari zinapoondoka katika maegesho, kwa kutokuwepo eneo hilo au kufanya mambo mengine nje ya kazi zao. Hali hii inawaongezea wananchi bili kubwa ambayo haifanani na muda walioegesha gari zao kwa vile bado watakuwa wanahesabika kwenye mfumo kuwa wapo kwenye maegesho ilhali wameshaondoka muda mrefu.

(a) Kwa kiasi gani Serikali inaifahamu changamoto hiyo.

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha mifumo hiyo inakuwa fanisi katika kufanya kazi zake na kujiepusha zaidi kutegemea watu ambao wanaisababishia mifumo hiyo kutoa taarifa zisizo sahihi na kupelekea kuwahujumu wananchi.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

51. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Taasisi mbalimbali zinazohusiana na usafiri wa vyombo vya moto vya barabarani hufanya ukaguzi wa vyombo (vehicle inspection) hivyo mara kwa mara.

Je, kaguzi hizo zinazofanywa zinaleta ufanisi au tija gani.

99. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nane kwa ujenzi wa *fly-over* mbili ikiwa ni kwa mara ya kwanza hapa Zanzibar. *Fly-over* ya Mwanakwerekwe, imeshakamilika na kuanza kutumika, kwa lengo la kuvusha gari zinazotoka barabara ya Kiembesamaki kuelekea barabara ya Amani. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vimekuwa haviitumii njia hiyo na kutumia njia ya chini.

(a) Je, Serikali imeshatoa elimu juu ya matumizi sahihi ya *fly-over* hiyo.

(b) Je, ni hiari au lazima kwa vyombo vya usafiri kutumia *fly-over* badala ya njia ya chini.

120. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Ninaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga barabara katika Jimbo la Tumbe. Hata hivyo, hadi hivi sasa barabara hizo hazijawekwa taa za barabarani.

Je, ni lini Serikali itaweka taa za barabarani kwenye barabara ya Shumba Vyamboni, Bule Kizota na Tumbe Soko la Samaki.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

23. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa mahitaji ya huduma za wagonjwa kuwekea maji (drip) ni makubwa na gharama za kununua huduma hiyo ni kubwa. Na kuwa katika kupunguza gharama za huduma za “oxygen”, Serikali imejenga mtambo wa kutengeneza “oxygen” baada ya ushauri uliotolewa na wadau mbalimbali akiwemo Mwakilishi anaeuliza swali hili.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kutengeneza “drip” ili kupunguza gharama kubwa za upatikanaji wa huduma hiyo.

(b) Je, ujenzi wa kiwanda hicho kwa makisio unaweza kuhitaji kiasi gani.

131. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Naipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa inaoufanya katika Sekta ya Afya, hasa ujenzi wa hospitali. Hata hivyo, baada ya Serikali kuweka Waendeshaji katika hospitali za Mikoa na Wilaya, Waendeshaji hao wamekuwa wakiajiri Madaktari Bingwa (Specialist) na Bingwa Mkuu (Super Specialist) mbalimbali kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika hospitali hizo.

(a) Je, Madaktari Bingwa na Bingwa Mkuu wangapi wameajiriwa na Waendeshaji hao.

(b) Je, ni kada zipi Madaktari Bingwa na Bingwa Makuu hao walizoajiriwa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga Upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa Madhumuni ya Kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**(Ramadhan Khamis Juma)**
**KAIMU KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**

**Zanzibar,**
**09 Septemba, 2026.**